

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

**MKOA WA DODOMA**

Tel.: 2354817/2321550  
Fax: 2321550



Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji  
S.L.P.1249  
**Dodoma**  
Barua pepe: [cd@dodomacc.go.tz](mailto:cd@dodomacc.go.tz)

Tarehe: 26/08/2019

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU UTIAJI SAINI MIKATABA YA UJENZI  
WA MAJENGO MAWILI YA VITEGAUCHUMI JIJI LA DODOMA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, anawatangazia wananchi wote kuwa kesho tarehe 27/08/2019 litafanyika zoezi la utiaji saini mikataba ya ujenzi wa majengo mawili ya vitegauchumi vya Jiji.

Mkataba wa kwanza ni ujenzi wa **Hoteli ya Jiji la Dodoma** (Dodoma City Hotel) katika Mtaa wa Nyerere. Mkandarasi ni Stecol Cooperation (China) kwa gharama ya mradi Sh. Bilioni 9.995.

Mkataba wa pili ni ujenzi wa **Jengo la Kitegauchumi cha Jiji** (Government City Complex) katika mji wa Serikali Mtumba. Mkandarasi ni Mohamed Builders Ltd (Tanzania) kwa gharama ya mradi Sh. Bilioni 59.3.

Mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), **Mhe. Seleman Said Jafo (Mb)**.

Zoezi hilo la wazi la utiaji saini Mikataba ya ujenzi wa vitegauchumi litafanyika katika viwanja vya **Nyerere Square** Jijini Dodoma, kuanzia Saa 4:00 asubuhi.

Ujenzi wa vitegauchumi hivyo utatumia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji.

Wananchi wote mnaalikwa kushuhudia tukio hilo la kihistoria.

Limetolewa na:

Joseph E. Fungo  
Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na UHUSIANO  
Halmashauri ya Jiji  
**DODOMA**